



**TUME YA
KUDHIBITI
UKIMWI
TANZANIA**

TACAIDS HABARI

**DKT. MRISHO APOKELEWA
OFISI ZA TACAIDS, DODOMA**

**Toleo Na. 003 | Januari – Aprili |
Mwaka 2025/26**

Zarida Mtandao



DKT. MRISHO AKABIDHIWA OFISI RASMI NA KUFANYA KIKAO KAZI NA WATUMISHI WA TACAIDS

Machi 30, 2026

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) Dkt. Adam Joseph Mrisho amepokelewa rasmi na watumishi wa TACAIDS wakiongozwa na aliekuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Samwel Sumba ambapo pia makabidhiano ya ofisi ya-

Dodoma.

Sambamba na tukio hilo pia Dkt. Adam Mrisho amefanya kikao Kazi cha kwanza na watumishi wa TACAIDS na kutoa shukrani kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteua kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TA-

Aidha, ametoa hamasa ya uwajibikaji na kujituma kwa watumishi wa TACAIDS na kuisitiza kufanya kazi kwa ushirikiano.

Kwa upande wake Dkt. Samwel Sumba aliekua Kaimu Mkurugenzi Mtendaji ametoa shukrani kwa watumishi wa TACAIDS kwa ushirikiano waliompa katika kipindi cha uongozi wake.



Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imetumia fursa ya maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar (Zanzibar International Trade Fair - ZITF) kutoa elimu ya

nanchi. Maonesho hayo ya 12 yamefunguliwa rasmi Januari 7, 2026 na Makamu wa pili wa Rais Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla katika viwanja vya maonesho Dimani Mkoani Magharibi Zanzibar na kuhudhuriwa na wadau kutoka ndani na nje ya

TACAIDS YAPANUA WIGO WA UTOAJI ELIMU YA VVU NA UKIMWI KUPITIA MAONESHU YA 12 YA ZITF

Januari 6, 2026



Akizungumza kwenye maonesho hayo Bi Naomi Mwakifamba alisisitiza kwamba elimu hiyo ya VVU na UKIMWI inalenga kuwasaidia Wananchi kujikinga na Maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI, kuondoa unyanyapaa na ubaguzi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU), kuhamasisha matumizi ya kipimo cha upimaji wa VVU binafsi cha Jipime na kuhamasisha ufuasi mzuri wa huduma za tiba na matunzo kwa WAVIU.



KIKAO CHA KAMATI NDOGO YA KITAIFA YA KONDOM

Januari 8, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - TACAIDS imeratibu Kikao cha Pili cha Robo ya Mwaka cha Kamati Ndogo ya Kitaifa ya Kondomu kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Kikao hicho kilifanyika Jijini Dodoma na kuwaleta pamoja wadau kutoka sekta mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa Serikali, Mashirika binafsi na washirika

wa maendeleo kujadili utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya upatikanaji na matumizi salama ya kondomu. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa robo

hine za ugawaji wa kondomu katika maeneo yenye vichocheo vya maambukizi ya VVU, Mikakati ya kuongeza upatikanaji wa kondomu katika maeneo ya vijijini

na mijini pamoja na Uhamasishaji wa jamii na vijana dhidi ya VVU na magonjwa ya zinaa. kuhusu matumizi sahihi ya kondomu kama njia ya kinga, Kamati imeahidi kuendelea kushiri-

hakikisha malengo ya kitaifa ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU na kulinda afya ya jamii yanafikiwa.



KAMATI YA KINGA DHIDI YA VVU KUIMARISHA MIKAKATI YA KINGA KWA VIJANA NA MAKUNDI MAALUM

Januari 9, 2026

Kamati ndogo ya kitaifa ya kinga dhidi ya VVU, chini ya uratibu wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), imefanya kikao maalum kujadili mikakati mipya ya kuimarisha kinga dhidi ya VVU kwa makundi rika ya vijana na jamii zilizo katika mazingira hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU

Katika kikao hicho, wajumbe walijadili kwa kina hali ya Wasichana balehe na Wanawake Vijana (AGYW) pamoja na Wavulana balehe na Wanaume vijana (ABYM), wakisisitiza umuhimu wa kuendelea kuwashirikisha katika kampeni za kitaifa za kinga na elimu ya afya ya uzazi.

Kikao hicho kilihusisha Asasi za kiraia na mashirika ya vijana, ambayo yamekuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU pamoja na elimu ya kupinga unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU.

Kamati hiyo ilipata fursa ya kujadili kuhusu utoaji wa huduma za kinga, tiba na matunzo kwa makundi maalum yaani Key and Vulnerable Populations (KVP), ambayo yapo kwenye hatari kubwa zaidi ya kupata maambukizi ya VVU.

Hivyo kubainika kwamba yanahitaji huduma maalum za kinga, matibabu na msaada, ikiwemo upatikanaji wa dawa za kuzuia maambukizi, PrEP (Pre-Exposure Prophylaxis) na PEP (Post-Exposure Prophylaxis) ili kuhakikisha hakuna kundi linaloachwa nyuma katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.



TACAIDS YASHIRIKI MAONESHU YA WIKI YA HUDUMA YA FEDHA

Januari 9, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imeendelea kuelimisha wananchi kwa kushiriki katika maonesho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitai-fa yaliyofanyika jijini Tanga, chini ya kauli mbiu "Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii." Maonesho hayo ya

mezinduliwa rasmi na Maonesho hayo ya mezinduliwa rasmi na Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Deogratius Luswetula, jijini Tanga na kushiriki-sha wadau mbalimbali wa sekta ya fedha na maendeleo ya Jamii. Katika maonesho hayo, TACAIDS imeweka mkazo wa kuhamasisha wananchi kutumia huduma za VVU na

UKIMWI pamoja na elimu ya kujikinga namaambu-kizi ya VVU na kuimarisha mwitikio wa UKIMWI nchini. Kupitia maonesho haya, TACAIDS imeonesha dhamira yake ya kuende-wa maendeleo katika kui-marisha afya ya jamii, iki-sisitiza kuwa elimu ya fedha na afya ni nguzo muhimu za ustawi wa ki-jamii na kiuchumi.

TACAIDS YA KUTANA NA KAMATI YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI

Januari 24, 2026

Katika maonesho hayo, TACAIDS imeweka mkazo wa kuhamasisha wananchi kutumia huduma za VVU na UKIMWI pamoja na elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na kuimarisha mwitikio wa UKIMWI nchini. Kupitia maonesho haya, TACAIDS imeonesha dhamira yake ya kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuimarisha afya ya jamii, ikisisitiza kuwa elimu ya fedha na afya ni nguzo muhimu za ustawi wa kijamii na kiuchumi.

"TACAIDS kupitia mfuko wa Udhadini wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (ATF) kwa kushirikiana na Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu imeweza kuratibu uwepo wa akiba ya dawa za ARV'S kwa watumiaji mpaka June 2027 ambapo tunatarajia kuwa tumeshaongeza hazina hiyo" amesema Dkt Sumba. Aidha, Dkt Sumba alitoa ufafanuzi kuwa kupitia mwongozo uliotolewa na Shirika la Afya Duniani WHO matibabu ya Kufubaza Virusi vya UKIMWI bado yanatolewa kupitia Dawa za ARV'S kwa watumiaji na sindano inatumika kama kinga ya ugonjwa huo.



TACAIDS NA CHAWAMATA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA ZA UKIMWI KWA WAFANYAKAZI WA MALORI TANZANIA

Januari 29, 2026

Akiongea wakati wa kuchangia mada ya uwasilishaji mjumbe wa kamati hiyo, Mbunge wa Buchosa Mhe. Eric Shigongo amesema ili kusaidia harakati za kuimarisha Mwitikio wa

Serikali kuongeza vyanzo vya mapato katika mfuko wa ATF ili kuweza kufikia malengo ya kutokomeza ugonjwa wa UKIMWI ifikapo 2030.

Moja ya mikakati iliyowekwa na TACAIDS ni pamoja na kuongeza program za kuelimisha jamii katika masuala mtambuka yahasuyo UKIMWI ikijumuisha magonjwa hatarishi kama

Presha ambapo program hii kwasasa hutolewa kwa wamama wajawazito na wanaonyonesha.

Menejimenti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (CHAWAMATA) wamekutana kujadili namna bora ya kuimarisha utoaji wa

Tiba na Matunzo kwa Wafanyakazi wa Malori Tanzania.

Mkutano huo umefanyika jiji Dar Es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kiwango cha maambukizi ya VVU kwa Wafanyakazi hao kinapungua ikiwa pamoja na kuhakikisha Wafanyakazi kwenye

shi na maambukizi ya VVU wanapata huduma za matibabu na matunzo kwa wakati.



TACAIDS NA LATRA KUENDELEA KUIMARISHA UPATIKANAJI WA RASILIMALI ZA NDANI KUPITIA TOZO YA UKIMWI

Februari 2, 2026



Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imefanya mazungumzo na Mamlaka ya Kudhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI nchini kupitia Tozo ya UKIMWI (HIV Response Levy - HRL).

Tozo hiyo iliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2025.

Mazungumzo hayo yamefanyikajijini Dodoma katika Ofisi za LATRA

TACAIDS YAONGOZA KIKAO KAZI CHA WADAU WA MRADI WA DREAMS

Februari 3, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imeongoza kikao cha wadau wa mradi wa DREAMS kujadili namna bora ya utekelezaji wa mradi huo. Kikao

Dodoma kwa kuwaleta pamoja wadau kutoka Wizara za kisekta.

Mradi wa DREAMS ulilenga kusaidia vijana wa kike walioko kwenye mazingira hatarishi, umeonyesha mafanikio makubwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Songwe, Shinyanga, Kagera na Mwanza.

Aidha, Kupitia ushirikiano wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI,



TACAIDS, Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mradi umeweza kutoa fursa za elimu, afya na ulinzi wa kijamii kwa mabinti wadogo.

Vile vile, Serikali kupitia TACAIDS imejipanga kuhakikisha Vijana wanafikiwa na Huduma kwa ujumla. Uwekezaji katika vijana wa kike ni msingi wa kupunguza maam-

kuimarisha ustawi wa jamii.

Kikao hicho kilihitimishwa kwa wito kuhakikisha programu za vijana zinaendelea kuwa nguzo ya matumaini kwa mabintiwa Kitanzania.

TACAIDS NA WIZARA ZA KISEKTA WAJA NA MKAKATI WA KUPUNGUZA MAAMBUKIZI MAPYA YA UKIMWI KWA VIJANA.

Februari 4, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na wizara za kisekta, Jamii pamoja na waratibu wa masuala ya vijana katika Halmashauri za Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mbeya, Songwe na Iringa wamekutana kujadili namna ya kuandaa mpango mkakati

liano hayo yamefanyika jijini Dodoma yaki-lenga kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata mazingira salama na rafiki, yanayowawezesha kuepuka hatari zinazoweza kuongeza uwezekano wa maambukizi mapya ya VVU. Hatua hii ni sehemu ya jitihada za kitaifa za kupunguza maambukizi mapya na kuimarisha afya ya jamii kwa vizazi vijavyo. TACAIDS na wizara husika wamesisitiza kuwa vijana ndio nguzo ya taifa na wanapaswa

kupewa nafasi ya kushiriki kikamilifu katika kupanga na kutekeleza programu zinazohusu maisha yao.



Kupitia mpango huu, serikali inalenga kuimarisha elimu ya afya, kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki kwa vijana, na kuendeleza kampeni za uhamasishaji zinazojikita katika kujenga tabia salama.

Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na jamii, mpango huu unatarajiwa kuwa chachu ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU na kuimarisha ustawi wa vijana, huku ukitoa dira ya taifa katika mwikio wa UKIMWI wa muda mrefu.

HABARI PICHA

17 Februari, 2026



Watumishi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania TACAIDS, Idara ya Mwitikio wa kitaifa wa VVU na UKIMWI wamefanya kikao kazi kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa afua za VVU na UKIMWI kwenye sekta ya Umma na sekta Binafsi. Kikao kazi hicho kimefanyika jijini Dodoma katika Ofisi za TACAIDS ikiongozwa na Daktari Hafidh Ameir.



TACAIDS YAZAMIRIA KUIMARISHA MWITIKIO WA VVU NA UKIMWI KWA VIJANA

Februari 27, 2026

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) imeongoza kikao kazi kilichojumuisha Taasisi za kissekta kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Kisayansi katika mwitikio wa VVU na UKIMWI kwa Vijana utakao angazia masuala ya VVU na UKIMWI,

huduma rafiki kwa Vijana ikijumuishisha Vijana balehe.



Akizungumza kwenye kikao kazi hicho. Dkt. Magreth Kagashe Meneja wa Dawati la Vijana na Masuala Mtambuka amesema kongamano hilo la Kisayansi linalotarajiwa kufanyika mwezi Aprili, 2026 linalenga kuleta tija katika mwitikio wa VVU na UKIMWI hasa kwenye afua zinazowalenga Vijana na Vijana balehe.



TACAIDS YARATIBU KIKAO CHA KAMATI MAALUMU YA UKAGUZI

Machi 9, 2026

Kamati maalumu ya Ukaguzi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS imefanya kikao cha 55 ili kuwasilisha na kujadili taarifa ya ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2025/2026 iliyoanza Oktoba hadi Disemba 2025.

Kikao hicho kimefanyika mkoani Morogoro na kuhudhuriwa na Viongozi wa TACAIDS pamoja na Wajumbe wa kamati kutoka nje Taasisi.

Kamati imejadili utekelezaji wa mpango kazi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa mwaka 2025/2026. Pia kamati imetoa mpendekezo ya kutembelea Miradi inayotekelezwa na kuratibiwa na TACAIDS.



ATF YABORESHA MATUMIZI YA AFUA ZA UKIMWI



Machi 12, 2026

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Udamini wa Kudhibiti UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF), Sabasaba Moshingi ameongoza kikao cha bodi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma kwa lengo la kujadili utekelezaji wa shughuli za mfuko ili kuboresha huduma na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU pamoja na kuimarisha mwitikio wa UKIMWI nchini.



DKT. SUMBA AONGOZA KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI

Machi 16, 2026

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hiyo, Dkt. Samwel Sumba, ameongoza kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Iringa kwa lengo la kujadili na kuboresha hali ya utendaji wa taasisi.

Katika kikao hicho, washiriki walijadili kwa kina mikakati ya kuimarisha utendaji bora wa TACAIDS ili kuhakikisha masilahi endelevu ya taasisi na kuendelea kutoa mchango mkubwa katika mwitikio dhidi ya UKIMWI nchini, kikao hicho kimefanyika mkoani Iringa.

Aidha, kikao hicho kimepitisha rasmi mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/27, hatua muhimu inayolenga kuweka msingi thabiti wa utekelezaji wa majukumu ya taasisi kwa ufanisi zaidi.

Katika kikao hicho wakuu wa Idara, Viten-go na Waratibu wa Kanda wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - TACAIDS pamoja na wawakilishi wao waliwasilisha mapendekezo ya bajeti za Idara, Vitengo na Kanda kwa Mwaka wa fedha 2026/2027.



KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI YATEMBELEA KONGA ZA DAR-ES-SALAAM

Machi 19, 2026

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Johannes Lukumay, Machi 19, 2026 imefanya ziara ya kutembelea Mabaraza ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (Konga) katika Jiji la Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Kamati imeridhishwa na namna Konga zinavyojishughulisha na shughuli za ujasiriamali na kilimo, hatua inayochangia kupunguza unyanyapaa na kuimarisha maisha ya wanachama wake.

“Wanakonga nimefurahishwa mmeithibitishia dunia kwamba hakuna wa kunyanyapaliwa na mmeongea kwa sauti kubwa, mmejituma na mmefanya kazi nzuri sana,” amesema Dkt. Lukumay.

Kamati imependekeza bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali hao zisajiliwe ili kuongeza thamani na ushindani wa kibiashara.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Mhe. Ummy Nderiananga, aliwapongeza wanakonga na kuwataka kuongeza bidii ili kufikia malengo ya maendeleo, akisisitiza kuwa Serikali inaunga mkono jitihada hizo.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dkt. Samwel Sumba, alibainisha kuwa TACAIDS itaendelea kushirikiana na Konga kwa kutoa mafunzo mbalimbali ili kuwa mabalozi wa kupunguza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI.



Akisoma risala kwa niaba ya wanakonga, wakilishi wao alitoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake thabiti.

“Kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI kumechangia maendeleo ya kiuchumi,” amesema mwakilishi huyo.



KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI YAPITISHA MAKADIRIO YA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Machi 19, 2026

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imepitisha makadirio ya mpango na bajeti ya shilingi Bilioni 12, 681, 254, 681 ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Bajeti hiyo imewasilishwa tarehe 26 Machi 2026, na Waziri wa Afya Mhe. Mohamed Mchengerwa katika Ukumbi wa Bunge jijini Dodoma ambapo pia amewasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mara baada ya kujadiliwa na kupitishwa na wajumbe, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Dkt. Johannes Lukumay ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna inavyohakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi katika maeneo mbalimbali.

Vilevile, Mhe. Dkt. Lukumay ameeleza kuwa, Serikali imewekeza nguvu kubwa katika nyanja ya afya kwa kuboresha miundombinu ya afya kwani ndiyo mtaji wa maendeleo.

Aidha, Waziri wa Afya Mhe. Mohamed Mchengerwa ameahidi kufanyia kazi ushauri na maoni yaliyotolewa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ili sekta hiyo muhimu iwe imara na yenye matokeo chanya kwa wananchi katika maeneo yote nchini.





KONA YA ELIMU



MIRAJI R. MAMBO
Mkuu wa Kitengo cha Sheria - TACAIDS

IFAHAMU SHERIA YA UKIMWI

Sheria ya UKIMWI ni Sheria kuu inayoshughulikia mambo ya kuzuia na kudhibiti VVU na UKIMWI nchini Tanzania yaani (The HIV and AIDS Prevention and Control R.E. 2023) Sura Na.431.

Lengo la Sheria hii ni pamoja na kuzuia kuenea kwa VVU (Virusi Vya Ukimwi), kudhibiti afya ya umma, kulinda haki na ustahimilivu kwa watu wanaoishi na VVU(WAVIU),

bu, ushauri, na msaada kwa walioathirika.

Sheria hii pia inaweka vifungu vinavyohusiana na makosa na adhabu kwa vitendo vinavyokiuka masharti ya sheria kulingana na Sheria ya Virusi vya UKIMWI(VVU) na UKIMWI,

hayo ni pamoja Kosa la uenezi wa VVU kwa Makusudi yaani Sheria inasema ni kosa kwa mtu anayelenga kwa makusudi kuambukiza mtu mwingine VVU.

Na adhabu yake ni Kifungo cha sheria cha miaka 5 hadi 10 gerezani. Pia Mahakama inaweza kulazimisha malipo ya fidia kwa mtu aliyeathirika kama inataona inafaa.

Kosa la Kuvunja Kanuni za Usalama, Hii inahusiana na kutofuata taratibu zinazopunguza hatari ya kueneza VVU mfano kutokutumi ulinzi au kutofanya kazi kwa usalama katika

tenda vitendo vinavyokiuka kanuni za usalama vinaweza kusababisha kuenea kwa VVU.

Adhabu ya kosa hilo kwa mtu binafsi ni Faini ya kati ya Tsh 200,000 na Tsh 500,000 au kifungo cha miezi 3 hadi 6, au vyote na adhabu kwa kituo cha afya ni Faini ya kati ya Tsh 3,000,000 na Tsh 5,000,000. Kituo hicho kinaweza pia kutolewa leseni yake (kuli-pwa kutoka kwenye rejista ya vituo vya afya).

Kosa lingine ni kufichua taarifa za Afya bila idhini ya muhusika. Sheria inaweka wazi kwamba kuvunja usiri wa taarifa kuhusu hali ya afya ya mtu, hususan mgonjwa wa VVU ni kosa, hata kufichua kwa namna isiyo halali taarifa kuhusu hali ya VVU ya mtu na adhabu yake ni faini ya kati ya Tsh 500,000 na Tsh 1,000,000, au kifungo cha miezi 6 hadi 12, au vyote. Sheria zinazoweza kuhusiana na VVU ni pamoja na

Sheria ya kanuni ya adhabu (Penal Code, Cap. 16). Hata kama sheria hii haielekezi kwa undani kuhusu UKIMWI, ina kifungu kinachoeleza kuwa ni kosa kufanya kiten-do chochote kinachoweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa hatari kwa maisha, ikiwa mtu anajua au ana sababu ya kuamini kitendo hicho kitasababisha kuenea kwa ugonjwa huo. Hii inaweza kutumika kama chanzo cha ziada ikiwa mtu anafanya vitendo hatarishi bila kufuata tahadhari.

Sheria hii imeundwa kulenga kuzuia kuenea kwa VVU kwa njia ya elimu, matibabu na ufuatiliaji, Kulinda haki za watu wanaoishi na VVU dhidi ya ubaguzi na dhuluma na Kupiga marufuku vitendo vya uenezi wa VVU kwa makusudi.

Hata hivyo, kuna changamoto kama ufafanuzi wa "makusudi" unaweza kuwa mgumu kuthibitisha mahakamani, ugumu wa kulinda haki wakati huo huo kukabiliana na uambukizi kwa

wasi juu ya jinsi sheria zinavyoathiri haki za watu wanaoishi na VVU, hasa wana wake.

Sheria ya kuzuia na kudhibiti VVU na UKIMWI inatoa muundo wa kisheria wa kulinda afya ya umma na kudhibiti kuenea kwa VVU nchini Tanzania. Inataja makosa kama kuambukiza kwa

usalama, na kufichua taarifa za afya bila idhini, na inatoa adhabu kwa kila kosa. Pia, sheria nyingine kama Penal Code inaweza kutumika kuzuia vitendo vinavyoweza kusababisha hatari ya maisha kwa ujumla.



DKT. SAMWEL SUMBA
Mkurugenzi Ufuatiliaji wa Mwenendo wa UKIMWI - TACAIDS

JUHUDI ZA TACAIDS KATIKA KUIMARISHA MWITIKIO DHIDI YA VVU NA UKIMWI NCHINI

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) ni Taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001.

Majukumu ya TACAIDS ni pamoja na kuratibu mwitikio wa kitaifa dhidi ya Virusi Vya UKIMWI, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mwitikio dhidi ya UKIMWI na kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya mwitikio dhidi ya UKIMWI hapa nchini. Aidha, TACAIDS ina jukumu la kusimamia Sera, Mikakati na

UKIMWI pamoja na kuimarisha ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kudhibiti UKIMWI kwa kuimarisha huduma za kinga, matibabu na matunzo kwa muktadha wa kutokomeza UKIMWI kama janga la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Rais wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imepata mafanikio makubwa katika kuimarisha mwitikio dhidi ya UKIMWI. Miongoni mwa mafanikio hayo ni Kuongezeka kwa kiwango cha watu wa-

kutoka asilimia 91 mwaka 2024 hadi asilimia 92 mwaka 2025, Kuongezeka kwa Watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU) wanaotumia dawa za kufubaza VVU (ARV) kutoka asilimia 98 mwaka 2024 hadi asilimia 98.5 mwaka 2025, Kuongezeka kwa WAVIU wanaotumia dawa za ARV ambao wamefubaza VVU kutoka asilimia 97 mwaka 2024 hadi asilimia 98.1 mwaka 2025.

Kuongezeka kwa idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo kwa Watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU) kutoka vituo 7,805 mwaka 2024 hadi 8,203 mwaka 2025. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za VVU na UKIMWI zinapatikana kwa urahisi kwa wananchi.

Aidha, kuimarika kwa huduma za VVU na UKIMWI hapa nchini kumepelekea kuenyelea kupungua kwa maambukizi mapya ya Virusi Vya UKIMWI toka zaidi ya watu 150,000 kwa mwaka mwanzoni mwa mwaka 1990 hadi kufikia watu 43,000 mwaka 2025. Hali kadhalika, vifo na maradhi yatokanayo na UKIMWI viendelea kupungua toka zaidi ya watu 100,000 mwaka 2000 hadi kufikia watu 24,000 mwaka 2025.

Sambamba na mafanikio haya, ili kuhakikisha huduma za VVU na UKIMWI zinaendelea kupatikana kwa wananchi, kupitia Mfuko wa udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) zaidi ya shilingi bilioni 400 zinatarajiwa kukusanywa toka vyanzo vya fedha vya ndani na kugharamia

Ili kudhibiti UKIMWI nchini, Serikali inaendelea kuwekeza katika huduma za kinga dhidi ya VVU katika makundi na rika zote ikiwa ni pamoja na vijana walio katika hatari kubwa wenye umri kati ya miaka 15 na 24, jamii za wachimbaji wadogowadogo wa madini, jamii za wavuvi,

marefu, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, watu wanaojidunga madawa ya kulevya na jamii nzima kwa ujumla. Elimu kwa jamii juu ya VVU na UKIMWI ni suala endelevu ili kudhibiti UKIMWI na kuondoa unyanyapaa ambao ni kikwazo kikubwa katika utumiaji wa huduma za VVU na UKIMWI kwa jamii.

